**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA UALIMU KINAMPANDA**

Tel.No:0763504238/0787412514
Mail: *kinampandatc@gmail.com*
Website: http/www.moe.go.tz
**Kumb. Na. KCCU/PS/A/III/2026/....**

S.L.P 532,
KINAMPANDA
**SINGIDA**
30.06.2026

**Ndg.………………………………………………….**
**S.L.P……………………………**
**……………………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU WA ELIMU YA AWALI MWAKA WA MASOMO 2026/2027.**

**UTANGULIZI:**

Napenda kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na **Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu *Elimu ya Awali*** katika **Chuo cha Ualimu Kinampanda**.

Mafunzo haya ya Ualimu ngazi ya Stashahada yatakuwezesha kutumia mbinu mbalimbali zitakazowawezesha watoto/Wanafunzi wa ngazi hii kujifunza kwa ufanisi. Mwelekeo wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni **kumwandaa mwalimu mahiri mwenye ujuzi stahiki katika Elimu ya Awali/Msingi**.

Aidha, mafunzo utakayopata yatakupatia sifa na ujuzi wa kufundisha hapa **Nchini** na **Nchi za nje** kwa kuzingatia fursa za soko la ajira ndani na nje ya Nchi. Elimu ya Awali ni msingi mkuu katika utoaji wa Elimu na imepewa kipaumbele katika Sera ya Elimu na Mafunzo iliyoboreshwa mwaka 2014 toleo la 2023. **HONGERA SANA**.

Chuo kipo Mkoani Singida, Wilaya ya Iramba, umbali wa kilometa 67 toka mjini Singida, kufuata barabara iendayo Mwanza. Kutoka Singida utapanda mabasi yaendayo Kiomboi ambayo hupitia Kinampanda na ukitokea Mwanza utashuka njia panda ya Kinampanda (KITUSHA).

**DIRA YA CHUO:**

*KUWA CHUO CHENYE MAZINGIRA BORA YA KUANDAA NA KUENDELEZA WALIMU KITAALUMA NA KITAALAMU KWA MAENDELEO ENDELEVU YA TAIFA LETU.*

**MOTTO WA CHUO**: *ELIMU NI KAZI.*

**Shabaha ya Chuo:** *KUANDAA MWALIMU BORA MWENYE ARI NA UWEZO WA KUFUNDISHA SHULE ZA MSINGI.*

## 2. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA

Chuo kinachukua wanachuo wa

a) Stashahada ya Ualimu wa elimu ya awali kwa muda wa miaka mitatu
b) Stashahada ya Ualimu wa elimu ya awali miaka mitatu (3) **kwa njia ya masafa (Walimu Kazini)**

## 3. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

- Kama umekubali kujiunga na kozi hii katika chuo hiki huna budi kuzingatia na kufuata kanuni na taratibu za mwenendo bora chuoni. Kuwa na heshima, nidhamu na maadili ya Ualimu.
- Unatakiwa kutumia hekima na busara katika maamuzi yote utakayoyafanya ukiwa hapa chuoni.
- Simu za mkononi **haziruhusiwi** kutumika katika vyumba vya madarasa, mitihani, wakati wote wa masomo ya jioni (Prep), mikutanoni na katika shughuli zote rasmi za chuo. Ukibainika unatumia simu katika maeneo hayo utanyang'anywa, utapewa adhabu kali na utarudishiwa mwisho wa muhula.

## 4. MASHARTI YA USAJILI

Ili uweze kusajiliwa unatakiwa utekeleze yafuatayo:

- Unatakiwa ulete c**heti chako/vyeti vyako halisi (Original certificate/s)** vya kufuzu mtihani wa kidato cha sita (**ACSEE}** au Result Slips kama cheti/vyeti havijatolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania au vyeti vya UALIMU (GATCE). Na Vyeti vya kuhitimu Elimu ya Sekondari **(leaving certificate)**.
- **Ulete nakala (**(Photocopy) ya cheti cha kuzaliwa. Ikibainika kuwa umeleta vyeti vya kughushi au cha mtu mwingine utashughulikiwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria za nchi.
- Unatakiwa kuripoti chuoni tarehe **15.08.2026 na** usipofika hadi tarehe **30.08.2026** utakuwa umejikosesha nafasi hiyo mwenyewe.
- Usajili utafanywa katika mfumo wa usajili kwa njia ya kielekroniki kabla ya kuja chuoni na utakapofika chuoni pia unapaswa kuripoti katika Ofisi ya Msajili wa Chuo ambapo vifaa vyote ulivyoagizwa vitakaguliwa.
- Ni kosa kwa mwanachuo kutosajiliwa mara baada ya kufika katika eneo la Chuo.
- Unatakiwa kuweka nakala za vyeti na taarifa zako zote katika file moja na kuliwasilisha ofisi ya usajili kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zako.

**ADA NA MICHANGO**

**(i)** **ADA:** Ada ya chuo ni Tshs. **450,000/=** kwa mwaka na italipwa kwa Mfumo wa malipo ya Serikali (**GEPG)** baada ya kupewa **Namba ya kuruhusu malipo (Control Number) ambayo utatengenezewa kwenye mfumo wa usajili wakati unapojisajili kabla ya kuja chuoni. Aidha, kama utapata changamoto yoyote Piga simu Na 0759297294 au 0672235535** kupata msaada zaidi.

**(ii)** **MICHANGO MINGINE**

Michango yote ifuatayo ilipwe kupitia Akaunti ya Chuo '**Kinampanda College of National Education', NMB Kiomboi Acc. No. 50602300001** na uje na risiti halisi ya michango uliyolipia Benki (Bank Pay in Slip). Michango hiyo ni kama ifuatavyo;-

- Fedha ya huduma ya kwanza ni Tshs. 10,000/= kwa mwaka.
- Mchango wa michezo Tshs.30, 000/= kwa mwaka.
- Mchango wa Ulinzi Tshs 30,000/= kwa mwaka
- Mchango wa Usajili na Kitambulisho ni Tshs 20,000/= kwa mwaka.
- Mchango wa ukarabati endelevu Tshs. 25,000/= kwa mwaka.
- Godoro linakodishwa kwa Tshs.10, 000/= kwa mwaka.
- Mchango wa serikali ya wanachuo Tshs. 5,000/= kwa mwaka.
- Vifaa vya usafi wa mazingira ni Tshs 20,000/= kwa mwaka.

- Aidha, Mwanachuo anatakiwa kuja na kadi ya Bima ya Afya kama anayo na **kama huna utalipia mchango wa bima ya afya Tsh 50,400/= kwa mwaka.** Kila mwanachuo anapaswa kulipia mahafali ya chuo Tsh 20,000/= kila mwaka.

(III) Michango kwa Stashahada kwa njia ya masafa kwa walimu kazini

a) Mchango wa usajili 20,000/= kwa kila mwaka
b) Fedha ya huduma ya kwanza ni Tshs. 10,000/= kwa mwaka.
c) Mchango wa ufuatiliaji na uendeshaji wa mafunzo 40,000/= kwa mwaka
d) Mchango wa michezo Tshs.30, 000/= kwa mwaka.
e) Mchango wa ukarabati endelevu Tshs. 25,000/= kwa mwaka.
f) Mchango wa serikali ya wanachuo Tshs. 5,000/= kwa mwaka.
g) Vifaa vya usafi wa mazingira ni Tshs 20,000/= kwa mwaka.

**Jumla ya michango yote ni 150,000/= kwa mwaka**

**VITU MUHIMU**

**Mavazi**

Mwanachuo anapaswa kuvaa sare safi, zisizobana na nadhifu wakati wote akiwa chuoni

(i) Mwanachuo anapaswa kuwa na sare maalumu za michezo na zivaliwe wakati wa michezo.

(ii) Mavazi yatakayovaliwa na mwanachuo wakati wote Chuoni sharti yawe ya heshima, safi na yenye kuendana na masharti kwenye kanuni hizi.

(iii) Mwanachuo analazimika kuvaa sare kamili ya Chuo wakati wote na mahali popote (ndani na nje ya chuo) katika kipindi chote cha masomo (semista/muhula); isipokuwa wakati wa kazi za nje, nyakati za jioni baada ya masomo, au siku za mapumziko ndani ya chuo.

(iv) Mwanachuo anatakiwa kuvaa kitambulisho chake shingoni wakati wote awapo chuoni au nje ya chuo kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma.

**A. SARE KWA WANAUME**

- Suruali ya buluu nyeusi (darkblue) na nyeusi zenye marinda mawili yenye mkunjo chini (turn up). Suruali nyeusi itavaliwa siku za jumatatu hadi jumatano na suruali ya buluu nyeusi itavaliwa siku za alhamisi na ijumaa. Aidha, koti la suti lenye rangi sawa na suruali linaweza kuvaliwa. Suruali itavaliwa na mkanda mweusi.
- Shati liwe buluu bahari (light blue) mikono mirefu.
- Tai ndefu buluu nyeusi (dark blue) au nyeusi. Tai itavaliwa kuendana na rangi ya suruali.
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza (kufunika) kisigino kifupi. Viatu vitavaliwa na soksi ndefu nyeusi.
- Hairuhusiwi kuvalia suruali chini ya kiuno (mlegezo).
- Mwanachuo anapaswa kuwa na sare ya michezo ambayo ni tisheti nyeupe na ‘track suit’ ya buluu bahari. Sare ya michezo ivaliwe wakati wa michezo tu.
- Uvaaji wa jinzi, kaptula, bangili, cheni, vimodo, skafu, makobazi, vilaka, na pete (zisizo za ndoa) na vingine vinavyofanana na hivyo hauruhusiwi.

**B. SARE KWA WANAWAKE**

- Sketi rinda boksi ya buluu nyeusi (dark blue) na nyeusi zenye urefu unafika chini karibu miguuni na zisizobana. Sketi nyeusi itavaliwa siku za jumatatu hadi jumatano na sketi ya buluu nyeusi itavaliwa siku za alhamisi na ijumaa. Aidha, koti la suti lenye rangi sawa na rangi ya sketi linaweza kuvaliwa.

- ❖ Shati iwe ‘light blue’ mikono mirefu na tai ndefu ‘dark blue’ au nyeusi. Tai iendane na rangi ya sketi.
- ❖ Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza kisigino kifupi, na soksi ndefu nyeupe.
- ❖ Nywele zichanwe au zisukwe mtindo wa utii wa roda (twende kilioni) mistari mitano (5) hadi nane (8) au kubanwa kisogoni kwa kibanio cheusi.
- ❖ Mwanachuo atakayependa kujisitiri kwa vazi la hijab anaelekezwa kumwona mlezi wake wa kike chuoni au Mkuu wa Chuo kwa maelekezo bayana.
- ❖ Mwanachuo anapaswa kuwa na sare ya michezo ambayo ni tisheti nyeupe na ‘track suit’ ya buluu bahari. Sare ya michezo ivaliwe tu wakati wa michezo.
- ❖ Uvaaji wa nguo angavu, khanga, kitenge, kofia, kilemba, hereni, bangili, mkufu, shanga, pensi, sketi fupi, nguo zenye mpasuo unaozidi magoti, makobazi na pete (isipokuwa pete ya ndoa) hauruhusiwi.

**C: VIFAA VINGINE MUHIMU:**

- ✓ Daftari **12 KUBWA** (Counter book) na kalamu za kutosha.
- ✓ Rimu moja (1) ya karatasi (Photocopy paper size A4) **kwa kila muhula**.
- ✓ Mkebe wa Hisabati (Mathematical Instrument set).
- ✓ Shuka mbili (2) za rangi ya Bluu isiyo na maua (Plain Blue)
- ✓ Mto, Foronya ya rangi ya Bluu na Chandarua.
- ✓ Vyombo vya chakula vya udongo (Sahani, Bakuli, Kikombe) na Kijiko.
- ✓ Ndoo ya kutunzia maji ya ujazo wa lita 20 na ya lita 10.
- ✓ Njoo na kitabu kimoja cha somo lolote linalofundishwa shule za msingi
- ✓ Njoo na file 05 kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zako za masomo pamoja na taarifa zako za usajili

**NB:** Ada na michango ikishalipwa **hairudishwi** endapo mwanachuo ataacha, kuachishwa au kuahirisha mafunzo.

**AFYA YAKO**: Unapaswa kupimwa afya yako kwa Daktari wa Hospitali ya Serikali kabla ya kuripoti chuoni. Fomu imeambatanishwa. Mwenye afya inayohitaji chakula maalum (Special Diet) ni vyema asije chuoni kwani chuo hakitoi chakula hicho.

**WAGENI:**

Mwanachuo haruhusiwi kutembelewa na mgeni yeyote kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa, isipokuwa Jumamosi na Jumapili kuanzia saa 7.00 mchana hadi saa 10 jioni na siku za Sikukuu kuanzia saa 7.00 asubuhi hadi saa 10 jioni. Mgeni huyo awe ni Mzazi/Mlezi au Ndugu wa karibu wa mwanachuo na ajitambulishe kwa Uongozi wa Chuo kupitia Mkufunzi wa zamu au Ofisi ya Uadili ndipo akutane na Mwanachuo husika. Hata hivyo chuo hakina nafasi ya kulaza wageni wa wanachuo chuoni.

**MITIHANI:**

Chuo hutoa mitihani, unatakiwa ufaulu mitihani yote unayopewa. Chuo hakitasita kukurudisha kama utashindwa kufaulu mitihani inayotolewa.

**KANUNI ZA CHUO**

Mwanachuo afikapo chuoni atapatiwa kanuni za chuo, ambazo utatakiwa uzisome kisha uzifuate na kuzizingatia wakati wote ukiwa mwanachuo. Kama utaona huwezi kuzitekeleza, UNASHAURIWA KUAHIRISHA MAFUNZO.

**10. MENGINEYO**

**Kumbuka kuja na namba ya NIDA ni muhimu sana**

**Karibu Chuo cha Ualimu Kinampanda – Iramba – Singida.**

**JOSEPHAT KOHI SAMWEL**

**MKUU WA CHUO**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU KINAMPANDA
S.L.P 532 KINAMPANDA

Nakala kwa:-

Mkurugenzi, Elimu ya Ualimu,

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

S.L.P. 10,
**DODOMA**.

Mkaguzi Mkuu wa Shule, Kanda ya Kati,
S.L.P. 1373,
**DODOMA.**

Afisaelimu Mkoa,
S.L.P. 5,
**SINGIDA**

Mwenyekiti wa Bodi,
S.L.P. 45,
KIOMBOI

**PART A:** **KIAMBATISHO NA.2**

**GOVERNMENT OF TANZANIA REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

TO: The Medical Officer From: Kinampanda Teachers' College
……………………………..
……………………………..

Please examine the above named as to his /her physical and mental fitness for a full time teachers course.
A: 1. (a) Eye – sight
2. Neuroses
3. Other serious Diseases B: blood group

Date……………………… Signature………………………………

Official Stamp

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE.**
(To be completed by Government Officer)
I have examined the above-named Student that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full-time teacher Education course.

- • (a) Eye – sight ………………………………………………
- • Hearing ……………………………………………….
- • Limbs ………………………………………………….
- • Speech ……………………………………………….
- • Leprosy ……………………………………………...

II. Neuroses …………………………………………………………
III. Other serious Diseases ……………………………………….
IV. Pregnancy …………………………………………………….
Date: …………………Signature: ………….................................